12. Huo unabii ulitimizwa? Luka 18:31-33, Mathayo 27: 29, 30, 41, 42.

    **Maelezo**. Kwa kweli unabii juu ya kuzaliwa na kifo cha Yahshua ulitimia kwa njia ya ajabu sana, ndio, hata kwa herufi. Tunayo hakika kwamba unabii kuhusu kurudi kwa Yahshua pia kutatimia hata kwa herufi.

**********************************

**Somo la Desemba 23, 2023 (Tevet 11, 5784).**

## JE, WATU WANAORUDI KATIKA NCHI TAKATIFU NI WAYAHUDI KWELI?

**Somo Kuu: Ezekieli 38: 14-23.**
**Fungu La Kukariri: Ezekieli 38:16.**

1. Ni baraka gani maalum ambayo Bwana aliahidi kwa Ibrahimu na kwa uzao wake, na ni laana gani iliyoahidiwa kwa adui wake? Mwanzo 12: 1-3,
2. Ni taifa gani la watu ambao wana cheti cha kisheria cha kurithi Nchi Takatifu? Mwanzo 15:18; 17: 8.
3. Je! Elohim amewafukuza warithi halisi wa nchi hii? Yer. 31: 35-37; Warumi 11: 1-4.



9. Je, unabii wa Zekaria kuhusu hatima ya watu ambao walimkataa na kumsulubisha mfalme wao ni upi? Zekaria 8:2, 6, 7, 11-15.
10. Mtume Paulo alinakili nini kuhusu tukio hili ambalo ni muhimu sana? Warumi 9:27, 28.
11. Ni zawadi gani itapeanwa kwa wale ambao wametiwa mafuta? Wagalatia 3:29; Ufunuo 21:3-5.
12. Ni jinsi gani tutakuwa na uhakika kuwa tutapata urithi huko? Ufunuo wa Yohana 21:7.

**********************************

**Somo la Novemba 4, 2023 (Cheshvan 20, 5784).**

## NUHU, MTU WA HAKI

**Somo Kuu: Mwanzo 6: 5-18.**
**Fungu La Kukariri: Waebrania 11: 7.**

1. Ni nani kati ya mababu za Nuhu alikuwa mtu mzuri kwa Elohim? Mwanzo 5: 21-32.

   **Maelezo**. Henoki alitabiri kuhusu mafuriko wakati alimwita mwanawe “Methusela”, ambalo linamaanisha “Wakati wa kifo chake, kutatumwa maji”. Methusela alikufa mwaka wa mafuriko.
2. Hali ilikuwa ipi katika nchi nyakati za Nuhu? Mwanzo 6: 5, 12.
3. Elohim aliamua kufanya nini kuhusu hili? Mwanzo 6: 7, 13, 17.





***"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao" Zaburi 122:6***



# Masomo Ya Bibilia

***kwa***

**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th day)**

Robo Ya Nne
2023

Ya
Oktoba, Novemba, Desemba.
**(Tishrei, Cheshvan, Kislev, Tevet)**

Watenda kazi wanahitajika,
Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568,**
**Jerusalem — Israel**

4. Kwa nini Nuhu hakuharibiwa? Mwanzo 6: 8, 18. Jadili mstari wa 9. Maana ya "kamilifu" ni kuwa takatifu.
5. Jadili juu ya ujenzi wa safina, masharti ambayo yalitumika kuijaza, na waliingia ndani yake.
6. Angalia sura ya 7: 5. Je! Hii ina maana yoyote muhimu?
7. Nini kilichotokea baada ya gharika kuisha? Mwanzo 8: 13-21.
8. Elohim alifanya ahadi gani? Mstari wa 22. Ni maagizo gani ambayo alipeana? Mwanzo 9: 1-7.

**********************************

**Somo la Novemba 11, 2023 (Cheshvan 27, 5784).**

## KUTHIBITISHWA KWA AGANO LA IBRAHIMU

**Somo Kuu: Mwanzo 49.**
**Fungu La Kukariri: Mwanzo 49:10.**

1. Ni nani ambaye Bwana alifanya naye agano hapo awali? Mwanzo 17:10.
2. Kwa wana kadhaa wa Abramu, ni nani ambaye agano lilifanywa imara tena? Mwanzo 26:24.
3. Ni nani ambaye Isaka aliabudu? Mwanzo 26:25.
4. Ni kwa maneno gani Bwana alithibitisha ahadi ya Ibrahimu kwa Isaka? Mwanzo 26: 3, 4.



**Somo la Desemba 16, 2023 (Tevet 4, 5784).**

## UNABII ULIOTABIRIWA NA KUTIMIA

**Somo Kuu: Isaya 53.**
**Fungu La Kukariri: Luka 18:31**

1. Ni katika maneno gani Musa alinena kuhusu Masihi? Kumbukumbu 18:15, 18, 19.
2. Ni jinsi gani tutajua kwamba nabii aliyenenwa na Musa ni Masihi? Matendo ya Mitume 3:20-24, 26.
3. Ni ishara gani ya ajabu nabii Isaya alitabiri? Isa 7:14
4. Unabii huu ulitimia? Luka 1:26-31, 2:7, Mathayo 1:22, 23, 25.
5. Ni eneo gani Masihi alikuwa azaliwe kwa mujibu wa Mika? Mika 5:2.
6. Unabii huu ulitimia?? Mathayo 2:1
7. Je, ni unabii upi kuhusu Yahshua unaopatikana katika Hosea? Hosea 11:1.
8. Jinsi gani unabii huu ulitimizwa? Mathayo 2:13, 14, 19-23.
9. Jinsi gani kuja kwa Masihi kulifaa kutangazwa? Isa 40: 3.
10. Ni kwa nani ambaye unabii huo ulikuwa utimie? Mathayo 3:1-3, Yohana 1:19-23.
11. Je, nabii alisema ni nini ingemtokea Masihi? Isa 53:7, 8



**Somo la Oktoba 7, 2023 (Tishrei 22, 5784).**

## MAJI YA UZIMA

**Somo Kuu: Isaya 55.**
**Fungu La Kukariri: Zaburi 46: 1.**

1. Ni ahadi gani ya Elohim kwa wale walio na kiu? Isaya 44: 3.
2. Ni matokeo gani itatokana na kumiminiwa roho? Mstari wa 4, 5.
3. Ni mwaliko gani mwingine unaotolewa kwa wale walio na kiu? Isaya 55: 1.
4. Ni himizo gani inayotolewa kwa wale wanaopoteza muda wao kwa kuishi katika dhambi? Mstari wa 2, 3.
5. Ni nini ingeweza kutokea ikiwa mwaliko huu ulikubaliwa na Israeli? Mstari wa 4, 5.
6. Ni ishara ipi inayotumiwa na Daudi kuelezea mwaliko huo? Zaburi 46: 4.
7. Yahshua alimpa mwanamke msamaria aina gani ya maji? Yohana 4:10.
8. Tofautisha maji ya kisima na yale ambayo Masihi Yahshua hutoa. Mstari wa 13, 14.
9. Siku ya mwisho ya sikukuu ya Wayahudi, ni mwaliko gani Yahshua aliwaitia, na bado huwaitia wote? Yohana 7:37, 38.
10. Je! Maji haya hutekwa na nini? Isaya 12: 3.

**********************************

4. Je! Musa alitumiaje kipindi cha pili cha maisha yake, na kiliishaje? Kutoka 3 na 4
5. Musa alianzaje kazi yake kama kiongozi wa Israeli? Kutoka 4:29 -31; Kutoka 5.
6. Musa aliwaongoza wana wa Israeli kwa muda gani? Kumbukumbu la Torati 2:7; 8:2, Hesabu 32:13.
7. Kwa nini basi, Wana wa Israeli walikaa miaka mingi jangwani wakati safari ya kwenda nchi ya ahadi ingewachukua siku 40 badala ya miaka? Hesabu 14:1-23,33-36
8. Je! Mwisho wa maisha ya kiongozi huyu mkuu ulikuwa upi? Kumbukumbu la Torati 34.

**Maelezo**: Maisha haya yamejawa na mambo yanayopingana - roho zinazopigana ndani ya mtu wa ndani. Na katika maisha haya, (tukichagua kufanya hivyo), tunaweza daima kupata kitu cha kunung'unikia au kulalamika. Hata hivyo, tumeumbwa kusifu na sio kunung'unika - kufurahi katika dhiki na kushukuru kwa mambo yote. Waefeso 5:20; Yakobo 1:2-4; Waebrania 12:2. Sisi ni dhahabu, (kama ilivyokuwa), iliyosafishwa katika moto - tukikamilishwa. Hebu, kila mmoja wetu, aweke **TUMAINI LAKE KWAKE!** Mithali 3:5.

**********************************



5. Kwa nini Elohim alithibitisha agano na Isaka? Mwanzo 26: 5.
6. Isaka alikuwa na wana wawili, ni nani ambaye alikuwa mbegu ya ahadi? Warumi 9: 10-14.
7. Ni kwa maneno gani Bwana alithibitisha agano na Yakobo? Mwanzo 28: 13-15; 35: 9-12.
8. Ni watoto wangapi waliozaliwa na Yakobo? Mwanzo 35:22.
9. Baraka za Yakobo juu ya wanawe kumi na wawili zilihusu matukio ya muda gani? Mwanzo 49: 1.

   **Maelezo**. - Ahadi zilizopitishwa kutoka kwa Abramu, kwa Isaka, kwa Yakobo, zimegawanyishwa kati ya wana kumi na wawili, pamoja na Yuda na Yosefu wakipokea ahadi zilizo kuu.

10. Mtoaji na Sheria na Mtawala (Mfalme) alikuwa atoke kwa kabila gani? Mwanzo 49: 9, 10.
11. Je, ni ahadi gani za kipekee katika agano la Ibrahimu? 22:17, 18.

**********************************



wanaoteseka kulileta machozi kwa macho yake, huruma kila mara iliambatana na uweza.

11. Jinsi gani alijibu mashtaka yaliyotolewa na Mafarisayo? Mathayo 12:24-30; Luka 11:15-23.

    **Maelezo**: Baba wa Mbinguni hutumia watu mwanga, kwamba njia zao mbaya ziweze kurekebishwa, lakini wakati muale mmoja wa nuru unakataliwa, mtazamo wa kiroho unaathiriwa kiasi, na kufunuliwa kwa nuru mara ya pili kunaeleweka kidogo. Kisha giza huongezeka polepole na kukaa.

12. Ni onyo gani alitoa kuhusu kukataa nuru, na kunena neno juu ya Roho Mtakatifu? Mathayo 12:31-32; 2 Wathesalonike 2:10-12.
13. Nini kilichosemwa kuhusu maneno mabaya, maneno mazuri, na pia maneno yetu katika siku ya hukumu? Mathayo 12:34-37.

**********************************



**Somo la Oktoba 14, 2023 (Tishrei 29, 5784).**

## NJIA, KWELI NA UZIMA

**Somo Kuu: Isaya 59: 1-16.**
**Fungu La Kukariri: Isaya 53: 6**

1. Ni hali gani iliyokuwa kabla ya Masihi kuja ambayo ni sawa na ile ya leo? Isaya 59: 2,3
2. Kulikuwa na mwombezi? Mstari wa 16.
3. Je! Kweli na haki inaweza kupatikana katika wakati huo? Mstari wa 14, 15.

   **Maelezo**: Ukweli na haki zinahusiana sana, kwa maana hakuna haki bila ukweli, na ukweli hauwezi kushushwa.

4. Je! Hali hiyo ilirekebishwa na nani? Mstari wa 16, sehemu ya mwisho, na aya ya 17.
5. Je! Ni mambo gani ambayo Baba alimtuma Masihi ulimwenguni? Isa. 61: 1, 2.
6. Je! Masihi alipokuja alizungumza kujihusu? Yohana 8:17, 18.
7. Ni nani aliyetoa ushuhuda maalum kwamba alikuwa Mwana wa Elohim? Mt. 3:16, 17.

   **Maelezo**: Wengine wanasema kwamba hakuwa Mwana wa Elohim, lakini kwa kudai hivi wanamkataa Baba kwa sababu alisema kutoka mbinguni: "Huyu ni Mwanangu

Somo La Novemba 18, 2023 (Kislev 5, 5784).

## DAUDI KUTIWA MAFUTA AWE MFALME

**Somo Kuu: 1 Samweli 16**
**Fungu La Kukariri: 1 Samweli 16:13.**

1. Ni swali gani Bwana aliuuliza, wakati Samweli aliomboleza kwa ajili ya Sauli? 1Samweli 16:1.

   **Maelezo**: Kila mtumishi wa kweli katika umri wote ana huruma. Ni moyo mwovu ufurahia juu ya yule huanguka. Paulo anasema: wale ambao wana roho wanapaswa kurejesha wale walioanguka. Wagalatia 6:1. Samweli angefanya hivyo, lakini Elohim tayari alikuwa amemkataa Sauli. Uasi wa Sauli ulikuwa wa makusudi.
2. Jinsi gani Samweli alihisi kuhusu kumtia mwingine mafuta? Jinsi gani alishauriwa ili Sauli asimshuku? Mistari 2, 3.
3. Kufika Bethlehemu, jinsi gani alionekana? Ujumbe wake ulikuwa nini? Aya 4, 5.
4. Mtazamo wa nabii Samweli wa kwanza kwa Eliabu ulikuwa upi? Mistari ya 6, 7.

   **Maelezo**: Mipango ya kibinadamu na kazi za kudhania inadhoofisha uhai wa Kanisa leo. Mwenyezi Elohim ana mpango wa jumla kwa ajili ya mtu. Yeye anataka sisi tuingie ndani ya



Somo la 9, Desemba 2023 (Kislev 26, 5784).

## MUSA, MWENYE SHERIA

**Somo Kuu: Kumbukumbu la Torati 34:1-8**
**Fungu La Kukariri: Waebrania 11:24, 25**

**Maelezo**: Maisha ya Musa yaligawanywa katika sehemu tatu:
(1) - Katika nyumba ya kifalme Misri;
(2) - Jangwani kama mchungaji wa kundi la kondoo la Yethro;
(3) - Jangwani pamoja na Israeli.

Kila moja ya vipindi hivi vitatu ilikuwa miaka arobaini. Miaka themanini ya kwanza ya maisha yake ilikuwa katika maandalizi ya miaka 40 ya utumishi.

1. Jadili hali iliyowaleta wana wa Israeli Misri na kuwaweka utumwani. Mwanzo 41:54, 57; 42:5, 6; 45:16-18; Kutoka 1:7-14.
2. Musa, Mwebrania, alikujaje kuitwa mwana wa binti ya Farao? Kutoka 1:15-22; 2:1-10.

   **Maelezo**: Josephus anatuambia kwamba binti wa Farao alikuwa Thermutis, ambaye hakuwa na mtoto wake mwenyewe; kwamba Musa alilelewa kuwa mrithi wa Farao. Soma Waebrania 11:24-27.
3. Je! Maisha ya Musa yalibadilikaje, nayo yalikujaje? Kutoka 2:11-25



mpendwa ambaye nimependezwa naye." Mat. 3:17.

8. Kabla hajaja ulimwenguni ukweli ulikuwa umejifichwa, au angalau haukutambuliwa? Mat. 13: 34, 35; 1 Kor 2: 7, 8.
9. Ni ahadi gani maalum imepeanwa kwa masalio ya watu? Yohana 8: 31, 32.

   **Maelezo**: Mwokozi aliponya wagonjwa, akawapa kuona vipofu, na akafungua ufahamu wao, akawasamehe dhambi zao, akifariji mioyo yao kwa maneno ya Injili, Kwa kweli alikuwa Neno aliyefanywa mwili na nuru ya ulimwengu.

10. Je! Aliahidi kutuma nini katika mahali pake alipoenda na ni kwa kusudi gani? Yohana 15: 26, 14: 26, 27.
11. Ni nini kingine kinachosemwa juu ya ukweli kuwa mlinzi wetu katika siku za mwisho za hatari? Zaburi 91: 4
12. Ni nini kitatokea kwa watu ambao hawapendi kweli, na hawana hamu yake? 2 Thes. 2: 9-12.

*********************************



yake, na kazi yake, na kwa kuwa na maoni yetu wenyewe kuyapinga maneno yake.

5. Je, tendo ndogo jema letu laonekana vipi kwa Bwana? Mathayo 10:40-42.
6. Wakati Mitume waliporudi kutoka ziara yao ya kuhubiri walifanya nini na ni wapi wao walienda na kwa nini? Marko 6:30-32.
7. Ni mwaliko upi wa upendo na ahadi Yahshua awaitia wale waliolemewa na kusumbuka? Mathayo 11:28-30.
8. Ni muujiza upi wa ajabu, alitenda kuonyesha nguvu ambayo aliyokuwa nayo? Marko5:1, 8, 15.
9. Wakati mtu huyu alitaka kuandamana na Bwana, alimwambia huyo mtu ajitahidi kufanya nini? Marko 5:18-20.
10. Hali ya mtu mwingine aliyeletwa mbele ya Yahshua ilikuwa vipi, na matokeo yalikuwa yapi? Mathayo 12:22, 23.

    **Maelezo**: Hii ilikuwa kazi ya Mwokozi wetu, ambayo aliyoikabidhi kwa wawakilishi wake. Alielewa sheria takatifu ya mbinguni kwamba dhambi ni shina la maovu kama hayo, ambayo yeye aliyashambulia kwanza. Kazi yake ilikuwa kuweka asili ya binadamu huru kutokana na maovu yake mengi, kwa kutenda juu ya chanzo. Huruma yake na huruma ya kina kwa ajili ya

3. Ni kwa nini watu hawakujua Yahshua kama Masihi kupitia maarifa ya unabii huu, na wa manabii wengine? Isaya 6: 9-12.
4. Je! Isaya 53:1-3 inahusiana vyovyote na wazo hili?

   **Maelezo**. Isaya 53 ni unabii wa kipekee wa Masihi. Kwa ufupi lakini kwa uzuri hutoa jumla ya kazi Yake kama Mwokozi wetu, unabii kuhusu kukataliwa kwake na watu na mateso yake kwa kuzibeba dhambi zetu. Kusoma sura hii moja inapaswa kuwashawishi wale walio na shaka.
5. Jadili Isaya 53: 10-12.
6. Mstari wa 8 ulitimizwaje hasa?

   **Maelezo**. - Kulingana na mapokeo ya Rabbi, Isaya aliuawa akiwa na umri wa miaka 90, kutokana na amri ya Manase. Alikatwa vipande viwili kwa msumeno katika shina la mti. Inaaminiwa na baadhi ya wengine kuwa Waebrania 11:37 inahusu kifo chake.

**********************************



mpango wake, sio kujaribu kumwiingiza ndani ya mipango yetu.

5. Ni wana wangapi wa Yese walipitishwa mbele ya Samweli? Aya ya 10-12.
6. Je, Roho alishuka juu ya huyo mwana mdogo wa Yese baada kutiwa mafuta na Samweli? Mstari wa 13.
7. Ni nini ilisemwa kuhusu hali ya kiroho ya Mfalme Sauli ya baadaye? Mstari wa 14.
8. Jinsi gani Daudi aliishi "katika njia zake zote" mbele ya watu? 1 Samweli 18:14, 16.

   **Maelezo**: Licha ya chuki yote katika moyo wa Sauli na kusudi lake kumuua Daudi likiendelea kuwa lenye nguvu, Daudi bado aliendelea kuwa shujaa na alibakia mtumishi wa kweli kwa Elohim na mfalme.
9. Wakati Sauli alifanya jaribio lake la mwisho kumuua Daudi, tukio gani la ajabu lilitokea? 1 Samweli 26: 2, 7-12.
10. Ni maombolezo gani ya huzuni Daudi alifanya juu ya Sauli na Yonathani? 2 Samweli 1:23-27.

    **Maelezo**: "Enyi milima ya Gilboa, visiwepo juu yenu Umande wala mvua, wala mashamba ya matoleo; Maana ndipo ilipotupwa kwa aibu ngao ya shujaa, Ngao yake Sauli, pasipo kutiwa mafuta." Mstari wa 21.

**********************************



**Somo la Desemba 30, 2023 (Tevet 18, 5784).**

## WITO NA USHUHUDIAJI WA MITUME

**Somo Kuu: Mathayo 10.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 10:16.**

1. Ni nguvu ipi waliopewa Mitume? Mathayo 10:5-8.
2. Ni maagizo yapi ya kiujumla yalitolewa? Mathayo 10:9-16.
3. Yahshua aliwaambia nini kuhusu upinzani watakaokutana nao? Mathayo 10:17-31.

   **Maelezo**: Wavuvi hawa wasio na masomo na wasio na ujasiri kutoka Galilaya, wanaume wachache wadhaifu, walitumwa dhidi ya nguvu zote za Mataifa. Kutokana na haya kazi yao ilikuwa haiwezekani, lakini uwezo wa Mbinguni ulikuwa pamoja nao, na ahadi hiyo pia ni yetu leo, "... Tazama, mimi nipo pamoja nanyi daima, hata mwisho wa dunia. Amina." (Mathayo. 28: 20.)
4. Ni ahadi gani Mwokozi alipeana? Mathayo 10:32-39.

   **Maelezo**: Kuna njia nyingi za kumkana: kwa kusema maovu, na kufuata anasa za dhambi, na kukataa dhabihu na kujikana binafsi kwa ajilli



**Somo la Oktoba 21, 2023 (Cheshvan 6, 5784).**

## IBRAHIMU, RAFIKI WA ELOHIM

**Somo Kuu: Mwanzo 12: 1-9.**
**Fungu La Kukariri: Warumi 4: 3.**

1. Jinsi gani Ibrahimu alikuwa wa uzao wa Nuhu? Mwanzo 11: 22-26.
2. Jina lake lilikuwa lipi awali, na baba yake na ndugu zake walikuwa nani? Mwanzo 11:26, 27.
3. Jadili mistari 28-32. Kuna angalau onesho moja la umuhimu katika kila mstari.
4. Ni ahadi gani iliyofanywa kwa Ibrahimu? Mwanzo 12: 1-3; 6-7.
5. Ibrahimu alikuwa akishughulisha na nini wakati huu? 15: 1-5.
6. Mjakazi wa Sarai, Hagari, alizaa mwana, Ishmaeli, kwa Abramu. Hata hivyo, huyu hakuwa mrithi wake. Jadili sura ya 17: 1-22. Angalia mabadiliko muhimu katika majina ya Abramu na Sarai.
7. Mwanzo 17:17 inazungumzia umri wa Ibrahimu kama miaka 100, na Sara kama miaka 90 (mstari wa 21). Ni jaribu gani kubwa lilitokea kwa imani ya Ibrahimu baada ya kuzaliwa kwa Isaka? Mwanzo 22: 1, 2.
8. Ibrahimu alikuwa na uhusiano gani na Elohim? 2 Mambo ya Nyakati 20: 7; Yakobo 2:23.

**********************************

**Somo la Novemba 25, 2023 (Kislev 12, 5784).**

## NYUMBA YA DAUDI

**Somo Kuu: Zaburi 89: 1-37.**
**Fungu La Kukariri: Ufunuo 22:16.**

1. Daudi alikuwa wa kabila gani la Israeli? Mathayo 1: 3-6.
2. Ni nani aliyemtia mafuta kuwa mfalme wa Israeli? 1 Samweli 16:13; Zaburi 89:20.
3. Kwa sababu ya uaminifu wake, Bwana alimwahidi nini? 2 Samweli 7: 8, 12-16.
4. Je! Imeandikwa nini katika Zaburi kuhusu agano hili? Zaburi 89: 3,4,27,29.
5. Ikiwa kizazi chake kitatenda dhambi ni nini itakuwa matokeo? Zaburi 89: 30-32.
6. Je! Hii itamfanya Bwana mwema avunje agano lake? Zaburi 89: 33-34.
7. Agano hili kwa Daudi litaendelea hadi lini? Zaburi 89: 35-37; 139: 11,12.
8. Je! Atataka mwana wa kiume aketi katika kiti chake cha enzi? Yer. 33:21
9. Je! Agano hili lina uhakika gani? Yer. 33: 19-22.

**Maelezo**. Jua, Mwezi na nyota bado ziko kwenye anga, kwa hivyo lazima uzao wa Daudi uwe kwenye kiti cha enzi kila wakati.



10. Je! Ni wazao gani wa Daudi ambao watakaa kwenye kiti chake cha enzi? Mathayo 1: 1; Isaya 9: 6, 7.
11. Utawala wake utaendelea hadi lini? Luka 1: 31-33.
12. Je! Ufalme wake hatimaye utajumuishwa katika ufalme gani? 1Wakorintho 15:24; Zek. 14: 9.

**********************************

**Somo la Desemba 2, 2023 (Kislev 19, 5784).**

## ISAYA, NABII WA INJILI

**Maelezo**. Isaya alitabiri katika siku za Uzia, Yathamu, Ahazi na Hezekia, au miaka ya 758 hadi 698 B.C. Unabii wake kuhusu Masihi ni wa kushangaza sana. Karne saba kabla ya Masihi, usahihi wa kutimia ni ushuhuda bora wa Biblia kuwa imeandikwa kwa pumzi za Elohim.

**Somo Kuu: Isaya 55.**
**Fungu La Kukariri: Isaya 66:20.**

1. Katika Isaya sura ya 1-8, nabii anasimulia uzoefu mzuri. Je! Unaona chochote ndani yake ambacho kinaweza kuwa mfano kwetu katika zama hizi?
2. Je, Isaya alitabiri kuhusu kuzaliwa kwa Masihi? Isaya 9:6, 7; 11:1-5.



**Somo La Oktoba 28, 2023 (Cheshvan 13, 5784).**

## AGANO LA KIIBRAHIMU KUTIMIA

**Somo Kuu: Ezekieli 34:20-31.**
**Fungu La Kukariri: Wagalatia 3:7**

1. Licha ya uzao mwingi, nguvu nyingi na mali mingi, ni ahadi ipi muhimu sana ya Agano la Kiibrahimu? Mwanzo 22:18.
2. Ni kupitia nani ambapo mataifa yote yatabarikiwa? Mwanzo 22:18.
3. Hii agano ambayo upitia Isaka na Yakobo kwa Israeli ilirudiwa na manabii watakatifu. Ni kumbukumbu gani katika agano jipya inayohusu agano hii? Luka 1:54, 55, 72; Wagalatia 3:7, 8, 14, 16.
4. Yahshua Masihi aliitwa mfalme wa Israeli? Yohana 1:49; Yohana 12:13; Luka 1:32.
5. Ni kwa watu gani Yeye atatawala? Luka 1:33; Ufunuo 11:15.
6. Jinsi gani Ezekieli alielezea kuhusu utawala huu? Ezekieli 34:13; Ezekieli 34: 23-29; Ezekieli 37: 22-27.
7. Ni unabii upi wa Yeremia unaohusu jambo hili? Yeremia 3:14, 15; Yeremia 23:3, 4; Yeremia 31:31-34.
8. Maono ya Mika ni yapi? Mika 4:3.



4. Je, Bwana anakusanya taifa la watu kurudi katika nchi ya Israeli, wale ambao aliondoa huko? Jer. 32:37,
5. Katika kutawanywa katika miongoni mwa mataifa, je! Wangekuwa na sifa fulani ambazo wangejulikana kama Wayahudi? Isa. 61: 9.
6. Je, Baba wa Mbinguni anawarejeshea Wayahudi nchi yao wenyewe kwa sababu wanastahili, au ni kwa ajili Jina Lake mwenyewe? Eze. 36: 22-32.
7. Wakati atawapa moyo mpya na roho, nini kinasemekana juu ya nchi yenye ukiwa na miji ya kale? Mstari 34-36.
8. Wakati Urusi na satelaiti zake zitakuja kupigana na Yerusalemu, je, ni watu wa Israeli (Wayahudi) ambao watakuwa katika nchi hio au ni mataifa mengine? Eze. 38:14.
9. Je, vita hivi vitafanyika wakati gani, na vitafanywa dhidi ya nani? Mstari wa 16.
10. Wakati Bwana Elohim atakusanya mataifa ili kuyahukumu mbele ya Yerusalemu, hasa ni kabila gani la Israeli ambalo litakuwa limekusanyika Yerusalemu? Yoeli 3: 1, 2; 9-16.
11. Ni kabila lipi pia ambalo Zakaria alilihusisha na Yerusalemu wakati Bwana atapigania Israeli? Zak. 12: 2, 3.

**********************************